



Maelezo zaidi ya wazazi kuhusu mafunzo ya mbali Cajon Valley April 1, 2020

Habari za leo Familia za Cajon Valley,

Ni matumaini yetu kuwa ujumbe utawafikia mkiwa salama wakati tunapoanza safari ya mafunzo ya mbali. Lengo letu hapa Cajon Valley ni kuwasaidia wewe na mtoto wako katika kujifunza kwa pamoja, inayomaanisha kutumia kwa pamoja maarifa, ujuzi, uvumilivu na uelewa.

Bila ya kuchoka timu ya Cajon Valley inafanya kazi ya kupanga utaratibu wa mafunzo yambali ya mtoto wako. Mafunzo ya mbali yataanza tarehe 20/4/2020, baada ya likizo fupi kuanzia tarehe 6/4/2020 mpaka 17/4/2020.

Wakati tunapoanza utaratibu wa mafunzo ya mbali, lengo letu la kwanza kama walimu ni kurudisha mahusiano na kuunganishwa na watoto wenu tukitumia msaada na mbinu kwenye mtandao. Hii italetta changamoto mpya, lakini wafanyakazi na wanafunzi wa Cajon Valley wapo tayari kuyamudu. Toka 2014, tumekuwa tukitumia mfumo wa kufundishia wa kuchanganywa 1:1 hivyo basi walimu na wanafunzi wetu wameshazoea kujifunza na teknolojia. Tunategemea kufanya kazi kwa ushirikiano na nyinyi ili kufanikiwa wakati wa hii hali ngumu.

Tumetayarisha maelezo ya wazazi tukizingatia maswali yaulizwayo mara kwa mara.

Ni nani atakaye mwongoza na kumsaidia mwanangu katika mafunzo ya mbali?

Wakati mafunzo ya mbali yataanza hapo tarehe 20/4/20, mwanafunzi wako atapangiwa mwalimu/mshauri mmoja wa kufanya naye kazi

- Wanafunzi wa shule ya msingi (Darasa K-5) wataendelea kufundishwa na mwalimu wa darasa lao.
- Wanafunzi wa sekondari (Darasa 6-8) watapangiwa mwalimu mmoja wa ushauri. Mwalimu huyu ataungana, saidia na kuwaongoza wanafunzi kupitia mafunzo ya mbali. Mwalimu wa ushauri atakuwa ni mtu mnamjua ambaye wewe na mtoto mwanafunzi wako mnaweza kwenda yakijitokeza maswali, mkihitaji msaada au mwongozo, Wanafunzi wataungana pia na walimu wao wengine wa shule za sekondari kupitia maeneo ya msaada na fursa zingine za kujifunza.
- Walimu wa madara watafanya kazi pamoja na wafanyakazi wengine wa CVUSD kutoa msaada wa zaidi kwa wanafunzi.
- Wanafunzi wenye ulemavu, ambao wana IEP, watapata msaada wa ziada unaotolewa kupitia mshauri/meneja wa elimu maalum na watoa huduma wahusikao.

Je, mtoto wangu atapataje masomo wakati wa mafunzo ya mbali?

Kazi zote za wanafunzi zitatolewa kupitia Google Classroom au Seesaw (Pre-K / K). Kila wiki, wanafunzi watapewa orodha ya kucheza yenye kazi za shule "Playlist" kulingana na darasa walilopo, inayoitwa eLearning. Hutarajiwi kufundisha, bali hakikisha kuwa mtoto wako ana muda na nafasi aliyoweka kando ili kumaliza kufanya kazi hii kila siku. Fikiria hii kama kazi ya ziada ya nyumbani, ila tu imeongezeka. Ikiwa mtoto wako ana IEP, mwalimu wa elimu maalum atakuwa



akifanya kazi na mwalimu wa darasa kuhakikisha kwamba shughuli zinapatikana kwa ajili ya mtoto wako na zitamfaa au kurekebisha pale itakapohitajika.

Muda gani wanafunzi wanapaswa kufanya kazi kwenye orodha za masomo?

Kutatolewa kazi ya takribani masaa mawili na nusu kila siku. Walimu wanaweza kurekebisha kulingana na mahitaji ya kila mwanafunzi. Orodha za kucheza za masomo zimetengenezwa kuainisha muda wa kukaa mtandaoni na wa kukaa nje ya mtandao, pamoja na shughuli rahisi za kimwili, na shughuli za sanaa ambazo wanafunzi wanaweza kushiriki nyumbani ili kujiongezea kwenye mafunzo yao.

There will be approximately two and a half hours of assignments provided each day. Teachers may make adjustments based on individual student needs. Playlists are designed to balance on and off screen time and include simple physical activities and art based activities that students can participate in at home to enhance their learning.

Ni aina gani ya masomo yatakayojumuishwa kwenye orodha ya masomo ya kila wiki?

Orodha za wiki zitajumuisha:

- Sanaa ya Lugha
- Hisabati
- Sayansi
- Masomo ya kijamii
- Masomo ya Kimwili / Harakati
- Kujifunza Hisia kwa Jamii
- Maendeleo ya Kazi
- Sayansi ya Kompyuta
- Sanaa ya Kuonekana na Kuigiza
- Ujumbe wa maonyesho

Kwa kuongezea, mipango kadhaa ya kurekebisha itasaidia mtoto wako kulingana na ujuzi wao wa sasa. Wakati wanafunzi wanapofanya kazi mtandaoni, programu hizi hutoa msaada zaidi au changamoto kulingana na majibu.

- iReady- Sanaa ya Lugha ya Kiingereza
- Achieve3000- Sanaa ya Lugha ya Kiingereza
- iReady- Hisabati
- ST Math- Hisabati
- Imagine Learning (ILE) - Upataji wa lugha

Wanafunzi wenye ulemavu, ambao hawawezi kupata programu na shughuli kwenye orodha ya kucheza, wanaweza kupangiwa programu au mtaala mbadala. Walimu wa elimu maalum na watoa huduma husika watakuwa wakibadilisha orodha ya kucheza, kila inapohitajika, kwa wanafunzi maalum.























Mbali ya programu hizi, walimu watapatikana mtandaoni muda wote wa wiki kusaidia wanafunzi kujifunza na kutoa msaada pale unapohitajika.

Zaidi ya programu hizi zinazoweza kubadilika, walimu watapatikana mtandaoni kwa wiki nzima kusaidia wanafunzi kwa kujifunza na kutoa msaada ambao wanaweza kuhitaji. Wanafunzi na



wazazi wanaweza kutuma barua pepe kwa walimu wakati wowote wakiwa na maswali au maombi maalum. Wafanyikazi pia watotoa masaa ya ofisi kukutana mtandaoni kupitia Zoom, chombo chetu cha mkutano wa video cha wilaya. Mikutano ya mtandaoni inaweza kupangwa kwa watu binafsi au vikundi vidogo.

Orodha ya kucheza inaonekanaje?

eLearning Playlist (Teacher Name) - Grade 3 Week of March 30th - April 3rd, 2020		
Weekly Assignments & Announcements (resources and directions) Please plan on spending 20 minutes per each activity per day. How do I login to HelloID? Teacher Welcome Video Virtual Spirit Days Big Idea:		
MONDAY	    	1. ELA: iReady Lesson HelloID 2. Math: Khan Academy HelloID 3. TEDxKids@ElCajon Talk & Prompt 4. Physical Education 5. Wellbeing Lesson
TUESDAY	    	1. ELA: Supplemental instructional video (You Tube?) + iReady Quiz HelloID 2. Math: iReady Lesson HelloID 3. Science: Mystery Science or Newsela-Science HelloID 4. Physical Education 5. Wellbeing Lesson
WEDNESDAY	   	1. ELA: Beginning Reading Poll & First read of Achieve article (complete ONE article) HelloID 2. Math: iReady Lesson HelloID 3. World of Work 4. Physical Education
THURSDAY	    	1. ELA: Reread Achieve article & complete activity (goal: 7 higher on the first try) HelloID 2. Math: Student Choice (ST Math or iReady Learning Game) HelloID 3. Social Studies - NewsELA HelloID 4. Physical Education
FRIDAY	  	1. Art 2. Computer Science 3. Physical Education Have a great weekend!

Itakuwaje mtoto wangu akihitaji changamoto au msaada zaidi kwenye masomo yake ya wiki?

Tafadhali tuma barua pepe kwa mwalimu wa darasa la mtoto wako (shule ya msingi) au mwalimu wa ushauri (shule ya sekondarii) ili kumwelezea au kutoa ombi lako.

Walimu watafanya kazi kurekebisha mipango ya kila wiki kadiri inayokidhi mahitaji ya mtoto wako. Ikiwa mtoto wako ana IEP, utakuwa na uwezo wa kumfikia mwalimu wa elimu maalum au wahusika wa utoaji huduma kwa msaada na namna. Namna na/au marekebisho ya mipango, ikiwa inahitajika, itafanywa katika orodha za kucheza kabla ya wanafunzi kupatiwa.

Nitazipata wapi wapi barua pepe za walimu na wafanyakazi wa shule?

Barua pepe zote za wafanyikazi zinapatikana kwenye ukurasa wa kwanza wa tovuti ya shule, chini ya kichwa, "Orodha ya Wafanyakazi". Wanafunzi wanaweza pia kutuma barua pepe kwa walimu moja kwa moja kupitia Google Classroom.



Wapi nitapata maelezo na rasilimali za ziada kwa wazazi?

Wazazi wanaweza tembelea www.cajonvalley.net/onlineresourcesparents kwa maelezo na rasilimali za ziada.

Wazazi wanaweza pia tembelea www.cajonvalley.net na bofya kwenye rasilimali za wazazi (Parent Resources).

Elimu maalum watatuma barua ingine itakayotoa maelezo zaidi kuhusu huduma na misaada wakati wa mafunzo ya mbali.

Orodha za kucheza zitatumwa lini?

Orodha za kucheza zitatumwa na mwalimu wa darasa , kila Jumatatu/siku ya kwanza saa tatu asubuhi

Mtoto wangu atapataje orodha yake ya wiki?

Wanafunzi wa darasa la 1-8 wataweza kupata orodha zao za kucheza za wiki kwenye Chromebook yao kupitia Google Classroom. Wanafunzi wa Pre-K na K wanaweza kupata masomo kupitia See Saw au Google Classroom. Kila mwalimu atawataarifu familia juu ya mbinu maalum ya kufundishia darasa lake.

Itakuwaje ikiwa Chromebook ya mwanangu ina hitilafu za kiufundi?

Shule zote zina siku na muda uliopangwa kushughulikia maswala ya Chromebook. Tafadhali wasiliana na msimamizi wa shule yako au mwalimu kwa maelezo zaidi.

Itakuwaje kama sina mtandao nyumbani kwa ajili ya mwanangu?

Maelezo juu ya mtandao wa bure na bei nafuu wa Cox yanapatikana katika <https://www.cajonvalley.net/Page/18150>

Ni kwa jinsi gani utampa maksu mtoto wangu?

Kwa wakati huu, ni muhimu kutambua kuwa wanafunzi hawagaiwa maksu kwa kazi zao za kila wiki. Badala yake, tutakuwa tunazingatia mfumo wa ukuaji, ambapo walimu hutoa maoni na maendeleo ya wanafunzi kwa kasi yao wenyewe. Tutabadilisha mbinu hii pale tutakapo pokea mwongozo na sera kutoka kwa viongozi wa serikali. Mpaka mapendekezo yabadilishwe, wafanyakazi watazingatia kutia moyo, msaada, na mwongozo. Hatuangualii kuwa wanafunzi wanamaliza kila kazi kila siku; tunangalia kuwa wanafunzi wanashiriki kwa masaa mawili na nusu yaliyogawanywa katika vipindi vinavyoeleweka kwa mtoto na familia. Tunataka wanafunzi wamalize kazi zao za kila siku kadiri ya uwezo wao wote na msaada wa mwalimu inapohitajika. Wanafunzi hawatazuiliwa kendelea au kuwekewa alama chini kwa kutokukamilisha kazi. Hizi ni nyakati ambazo hazijawahi kutokea, na walimu na familia wanafanya kila wawezalo kutoa elimu, mwingiliano wa kijamii, msaada wa kihemko, mwongozo, na huruma kwa namna ambayo inawapa motisha wanafunzi na kuhisi mafanikio.

Washauri wa shule watapatikana wakati wa mafunzo ya mbali?

Shule zetu zote katika Umoja wa shule wilaya ya Cajon Valley zinatoa ushauri kamili kwa wanafunzi wote. Washauri wa shule watapatikana wakati wa mafunzo ya mbali na maelezo ya mawasiliano ya mshauri wa shule wa mtoto wako yapo kwenye tovuti ya shule. Tutaendelea



kuungana na wanafunzi na kutoa msaada wa ushauri kupitia vituo vya ushauri mtandaoni. Cha nyongeza, unaweza kwenda moja kwa moja cajonvalley.net na bonyeza “Wasiliana na Mshauri (Contact a Counselor)” kwenye kurasa kuu. Tupo hapa kuwasaidia tafadhali jisikieni mpo huru kutufikia

Itakuwaje nikitaka kubadilisha maelezo yangu kwa ajili ya mawasiliano na wafanyakazi?

Ili mwalimu/mshauri wako aweze kukufikia, ni muhimu kuwa nambari zako za simu na barua pepe ni sahihi. Tafadhali rekebisha maelezo yako kwenye tovuti ya wazazi au tuma barua pepe kwa mwalimu mkuu wa shule na maelezo ya mawasiliano yako mapya.

Je, kutakuwa na kazi za shule wakati wa likizo fupi?

Hapana. Wanafunzi wanaweza kuendelea na masomo ya Achieve3000 na ST Math. Vifaa vya kuchapishwa vya i-Ready vinapatikana pia katika <https://www.cajonvalley.net/onlineresourcesparents>

Je, chakula kitaendelea kugaiwa wakati wa likizo fupi?

Ndio, ugawaji wa chakula utaendele Juamatatu/siku ya kwanza -Ijumaa/siku ya tano, wakati wa wiki mbili za likizo yetu fupi. Kwa sababu ya sikukuu, ugawaji hautofanyika ijumaa?siku ya tano, tarehe 10/4/20. Mwongozo umebadilishwa wazazi wanaweza sasa kuchukua chakula bila watoto wao kuwepo.

Nitapataje maelezo ya zaidi juu ca mafunzo ya mbali ya Cajon Valley?

Kila wiki familia itapata mawasiliano kwa njia ya barua pepe wakati wa kipindicha mafunzo ya mbali. Mawasiliano haya yatatoa fursa zinazoendelea za maelezo ya zaidi na rasilimali.

Majukumu ya kila siku ya mafunzo ya mbali

Jukumu la mzazi

1. Kumwandalia mwanao mahali pazuri pa kukaa na Chromebook yake iliyojazwa umeme. Ikiwezekana, toa nafasi iliyo tulivu na isiyo na usumbufu.
2. Hakikisha kuwa mtandao nyumbani kwako unafanya kazi.
3. Mhimize mtoto wako kwenye kufuatilia maanani masomo yake, apumzike inapohitajika, na kusaidia kutatua tatizo lolote kwa kumsaidia mwanafunzi wako kuwasiliana na mwalimu/mshauri wake.
4. Mhimize mwanao afanye vizuri, na huku ukizingatia ratiba yao ya kila siku.

Jukumu la mwanafunzi

1. Ingia kwenye Google Classroom
2. Tafuta orodha yako ya wiki kwenye Google Classroom
3. Bonyeza kwenye zoezi katika orodha na kamilisha kazi
4. Muulize mwalimu maswali kwa kutumia barua pepe na tafuta muda wa ofisi wa mwalimu



5. Jiunge na mwalimu katika makundi madogo ya Zoom wakati yanapotolewa au unapohitajika
6. Ulizia msaada kutoka kwa mwalimu/mshauri au mshauri wa shule inapohitajika
- 7.

Teacher/Advisors Role

1. Kuwafikia wanafunzi na kuwahakikishia kuwa wanapendwa, kuna misaada na hururma kutoka kwa walimu/washauri wao
2. Kutengeneza nakala ya wiki ya eLearning, kuibinafsisha kama itahitajika, na kufuatilia kuwa wanafunzi wameingia masomoni
3. Kuwa na masaa ya ofisi kwa ajili ya wanafunzi na wazazi
4. Kuendesha Zoom kwa mtu au kikundi cha watu inapohitajika
5. Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi na kurekebisha orodha ya masomo ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi kila wiki
6. Kuungana na wazazi ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanao muda, nafasi na vifaa vinavyohitajika kukamilisha kazi zao.